OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

SHULE YA SEKONDARI MAVALA
S. L. P 789,
NJOMBE.
01/12/2020

KUMB NA: MVLSS/LUD /JOIN.INS/VOL.1/2020/____

MZAZI /MLEZI WA .....
S. L. P .....
.....

YAH:MAAGIZO KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA (I) 2020

1. Nafurahi kukujulisha kuwa mtoto wako amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Mavala. Shule ya Sekondari Mavala ipo wilaya ya Ludewa, yapata kilomita 16 kutoka Kigasi kufuata barabara iendayo Milo.
2. Shule hii inatoa mafunzo kwa masomo yote ya sekondari (kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne) pamoja na mafunzo ya awali ya Kompyuta (Computer Application).
3. Pamoja na barua hii, ninaambatanisha yafuatayo;
   a. Maelekezo ya sare ya shule
   b. Sheria za shule na habari muhimu kwa kila mwanafunzi.
   c. Fomu ya kujiandikisha shuleni.
   d. Fomu ya ahadi ya mwanafunzi na mzazi/mlezi.

   Fomu (c) , (d) na medical examination zijazwe na kurudishwa shuleni
4. Mzazi/Malezi ripoti shuleni na mwanao mnamo tarehe 11/01/2021, mwisho wa kuripoti kwa hiari ni tarehe 15/01/2021. Baada ya tarehe hiyo utachukuliwa hatua za kisheria kwa kutomleta mwanao shuleni.
5. Ni matumaini yangu kwamba mwanao atanufaika na kufurahia maisha kwa muda wote atakaosoma hapa na ataonesha tabia njema, ari ya kujifunza kwa juhudi na maaarifa pamoja na ushirikiano na walimu, wafanya kazi wasio walimu na wanafunzi wenzake.

Hongera kwa kupata nafasi hii na karibu sana **SHULE YA SEKONDARI MAVALA.**

THE HEADMASTER
MAVALA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 789
NJOMBE

ISSA T. MLIGO
MKUU WA SHULE

1: MAELEKEZO YA SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE

Wavulana;

i. Suruali mbili za darasani dark blue (angalia kitambaa cha mfano ulichowekewa kwenye barua hii).
ii. Mashati meupe mawili mikono mirefu
iii. Viatu vyeusi vya ngozi (vya kamba) pea mbili
iv. Soksi nyeusi zisizo na rangi yeyote pea mbili
v. T-shirt nyekundu ya kazi isiyo na maandishi (aje nayo).
vi. Suruali nyeusi ya kazi
vii. Sweta la kufumwa rangi ya bluu iliyokolea (dark blue) aje nayo.

Wasichana;

i. Suruali mbili za darasani rangi ya bluu iliyokolea (dark blue) (angalia kitambaa cha mfano ulichowekewa kwenye barua).
ii. Visolo viwili vyeupe vyenye mikono mirefu inayoishia chini kidogo ya kiwiko na urefu ifike juu ya goti (mchoro umeambatanishwa)
iii. Viatu vyeusi pea mbili vya kamba na visivyo na visigino virefu **(viatu vya plastiki kama bajaji haviruhusiwi)**
iv. Soksi ndefu nyeupe pea mbili
v. Sketi moja ya kazi (rangi ya damu ya mzee).
vi. Sweta la kufumwa rangi ya blue iliyokolea (dark blue) aje nayo.

NB: SARE ZA KUBANA AU FUPI au ZILE ZILIZOMODOLEWA HAZITAKUBALIWA NA ZITANYANG'ANYWA, KILA MWANAFUNZI ANAPOKUJA KURIPOTI LAZIMA AWE AMEVAA SARE YA SHULE

2**. 0 ,MAHITAJI MENGINE**

Kila mwanafunzi aje na faili (flat file) mbili, moja litatunzwa shuleni

2.1 VIFAA VYA USAFI NA KAZI

i. Fagio moja (chelewa)
ii. wavulana jembe jipya lenye mpini wasichana kwanja moja
iii. Ndoo moja ya lita kumi (10)

NB: Vifaa hivi vyote vitatunzwa shuleni kwa utaratibu maalumu

2.2 **VIFAA VYA DARASANI**

i. Daftari kubwa tisa (09) **(kaunta(3 quire)**) kwa masomo yote
ii. Daftari ndogo tatu (03)
iii. Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set)
iv. Peni za bluu au nyeusi na kalamu za risasi za kutosha
v. Kamusi ya kingereza (English dictionary)

2.3 VIFAA VYA MICHEZO

i) Wavulana

a. Bukta b. T-shirt c. Raba za michezo d. Soksi za michezo

ii) Wasichana

a. Traksuti za michezo b. T- shirt za michezo c. Raba za michezo d. Soksi za michezo

3.0 MAHITAJI YA DAHARIA /(HOSTELI) WASICHANA /WAVULANA.

i. Godoro la futi mbili na nusu na blanketi mbili nzito
ii. Mshuka mawili ya rangi ya bluu bahali (wavulana)
iii. Mashuka mawili ya rangi ya pink (wasichana)
iv. Tranka moja na kufuli
v. Vyombo vya chakula sahani 1, kijiko 1, na bakuli 1, kikombe 1.

NB. Wanafunzi wote wa kike watatakiwa wakae hosteli ili kuboresha Taaluma yao na kuongeza ulinzi zaidi. Pia ni agizo la **MH: MKUU WA WILAYA YA LUDEWA**

3.1 SARE YA HOSTEL

i. Wasichana
   a. Sketi moja(01) za rangi ya light blue
   b. T-shirt moja (01) nyeupe zisizo na maandishi
   c. Tracksuit nyeusi
ii. Wavulana
   a. Suruali nyeusi moja (01)
   b. T- shirt nyeupe moja (01) zisizo na maandishi
   c. Tracksuit bluu bahali

4.SHERIA ZA SHULE NA MAAGIZO MUHIMU KWA WANAFUNZI

i) Mwanafunzi lazima awahi shuleni na kuwa popote anapotakiwa kwa shughuli za shule au kitaifa kwa wakati uliopangwa.

ii) Mwanafunzi atatakiwa kushiriki kwa makini kufanya masomo ya jioni (night preparation).

iii) Kutunza mali za shule.

iv) Utekelezaji; Mwanafunzi lazima atekeleze kwa ufanisi wa hali ya juu shughuli zote za shule atakazotakiwa kufanya katika mambo ya taaluma, nidhamu, usafi wa mazingira,kazi za shamba, utamaduni na michezo.

v) Adabu; Heshima na utii ni vitu vya lazima shuleni. Mwanafunzi lazima awe na adabu na kutii kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii nzima ndani na nje ya shule.

vi) Kuwa kimya; Ni marufuku kupiga kelele darasani au ndani ya eneo la shule. Mwanafunzi atatakiwa kuwa kimya pale atakapotakiwa kuwa hivyo.

Vii) Sare; Mwanafunzi lazima awe na sare safi za shule na **kuwa nadhifu muda wote**. Ni marufuku kuacha kifua wazi au kuacha shati ikipepea nje huria bila kuchomekea. Sare ya shule itavaliwa wakati wote mwanafunzi awapo shuleni hususani wakati wa;

a. Masomo darasani
b. Mwanafunzi anapotoka nje kwa shughuli za kishule
c. Mhadhara wa shule
d. Maandamano
e. Safarini, kuelekea/kutoka shuleni wakati wa likizo

viii) Usafi binafsi

Kila mwanafunzi lazima awe msafi mwili wake, nguo, nywele zake ziwe fupi na zichanwe, kofia na mapambo yoyote hayaruhusiwi wakati mwanafunzi akiwa shuleni.

ix) Ulevi wa aina yeyote kama vile kuvuta bangi, sigara, madawa ya kulevya au kileo cha aina yeyote ni marufuku kwa mwanafunzi

x) Umiliki wa simu au laini

Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu au laini, mwanafunzi mwenye shida ya kuwasiliana na mzazi/mlezi wake awapo shuleni atatumia simu ya shule/ ya mwalimu baada ya kuhakiki shida yake.

5.MAKOSA YA KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE

Makosa yatakayo mpelekea mwanafunzi kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule mara tu akibainika kuyafanya ni pamoja na;

I) WIZ1
II) KUJIHUSISHA NA MAPENZI IKIWA NI PAMOJA NA UASHERATI, UBAKAJI, USHOGA NA USAGAJI
III) ULEVI NA MATUMIZI YA MADAWA YA KULEVYA
IV) MAKOSA YA JINAI
V) KUPIGANA AU KUPIGA
VI) KUHARIBU KWA MAKSUDI MALI YA SHULE
VII) KUOA AU KUOLEWA
VIII) KUDHARAU BENDERA YA TAIFA
IX) KUPATA MIMBA AU KUSABABISHA MIMBA NDANI NA NJE YA SHULE
X) KUTOA MIMBA
XI) KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI
XII) KUMILIKI SIMU AU LAINI YA SIMU
XIII) KUVURUGA AMANI, KUCHOCHEA/KUSABABISHA AU KUONGOZA MGOMO SHULENI

6. TAARIFA MUHIMU KWA MWANAFUNZI

1. RUHUSA; Mwanafunzi anaposhindwa kuhudhuria masomo au shughuli nyingine za shule kutokana na ugonjwa au tatizo lolote anapaswa kuomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu.
2. VIRANJA; Mwanafunzi aliyechaguliwa kuwa kiranja atawajibika kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Kiranja ni kiongozi hivyo lazima awe mfano. Pia kiranja atatoa adhabu ndogondogo kwa mwanafunzi atakaevunja sheria na taratibu za shule kwa niaba ya mwalimu.
3. UGONJWA; Mwanafunzi anapokosa kuhudhuria masomo kwa sababu ya ugonjwa lazima awe na cheti cha daktari wa hospitali inayotambulika na ameomba ruhusa na kupata kibali. Vibali vya kwenda hospitali vitatolewa na mwalimu wa zamu.
4. MAHUDHURIO DARASANI; Mwanafunzi atatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani bila kukosa . Aidha mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje bila ruhusa ya mwalimu, endapo mwalimu wa somo hayupo wanafunzi watumie muda huo kujisomea na kukamilisha kazi zilizo tolewa. Walimu wa madarasa wakishirikiana na viranja wa madarasa watasimamia mahudhurio ya mwanafunzi darasani.
5. MATATIZO, SHIDA NA MAPENDEKEZO; Matatizo, shida na mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wanafunzi yatajadiliwa katika vikao halali kulingana na utaratibu wa shule(vikao vya darasa, bweni, n.k) nakufikisha kwenye halmashauri ya shule ambacho ni chombo cha kumtaarifu na kumshauri mkuu wa shule.

7. **MIPAKA**

Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali na sababu maalumu.

a. Nyumba ya mwalimu
b. Ofisi za walimu
c. Maabara
d. Vilabu vya pombe
e. Nyumba za starehe
f. Nyumba zaa kufikia wageni

8. **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOTAKIWA KUZINGATIWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI MARA AFIKAPO SHULENI.**

a) Fomu ya afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi afikapo shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu pamoja na malekezo mengine yatakayo tolewa shuleni.

TAFADHALI, SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

THE HEADMASTER
MAVALA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 789
NJOMBE

ISSA T. MLIGO

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA
SHULE YA SEKONDARI MAVALA

AHADI ZA MWANAFUNZI

(Ijazwe na kurudishwa kwa mkuu wa shule)

Mimi..... nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote ya sheria kanununi na taratibu za shule na nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mavala kuanzia tarehe .....hadi nitakapo hitimu kidato cha nne.

Kwahiyo naahidi kuwa;

a) Nitazitii sheria, kanuni na taratibu za shule na kutimiza mambo yote muhimu kama yalivyo tajwa.
b) Sitashiriki katika vitendo vyote ambavyo vitakuwa kinyume na maagizo ya shule pamoja na uongozi wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
c) Nitatunza mali ya shule ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu, vifaa vya kazi n.k
d) Nitashiriki kikamilifu katika shughuli zote za darasani, usafi wa mazingira, utamaduni, michezo na kazi zote za elimu ya kujitegemea.
e) Sitashiriki katika mgomo, kuchochea au kuongoza mgomo shuleni.
f) Sitamiliki simu au kutumia simu kinyume na taratibu ndani na nje ya mipaka ya shule.

....

Sahihi ya mwanafunzi **Tarehe**

AHADI YA MZAZI /MLEZI

Mimi.....mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……..... …….

Naahidi kwamba;

1. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule, walimu na wafanyakazi wengine wa shule katika kumlea na kumuelimisha mwanafunzi tajwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na kumtimizia maagizo na mahitaji yote muhimu yaliyotajwa.
2. Nitafanya kila niwezalo ili kumwazesha mwanangu kufika shuleni mapema (kuwahi shuleni), kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza kwa muda wote wa miaka minne.

....

Sahihi ya mzazi/mlezi Tarehe

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA
SHULE YA SEKONDARI MAVALA

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI

A. Jina la kwanza..... Jina la baba …….. Jina la ukoo…….
Jinsia (msichana/mvulana) ……
Dini .....
Tarehe ya kuzaliwa .....
Shule ya msingi aliyofanyia mtihani wa darasa la saba.....
Kama ulihamishwa kutoka shule nyingine ya sekondari; Jina na anwani ya shule hiyo .....
.....
…….....
B. Jina kamili la mzazi/mlezi.....
Anwani yake.....
Namba ya simu ya mzazi/ mlezi ..... no ya kitambulisho cha taifa……
(Ikiwa mzazi/mlezi atahama au kubadilisha anwani, taarifa itolewe mapema kwa mkuu wa shule)
Anatoka kitongoji cha ……kijiji …….. kata……..wilaya……
C.Jina la mama mzazi…….
Anwani yake ……..
Namba ya simu ya mama…….. no ya kitambulisho cha taifa……
Anatoka kitongoji cha ……kijiji …….. kata……..wilaya……

D. Jina la mwenyekiti wa kitongoji.....
Namba ya simu ya mwenyekiti wa kitongoji.....

TAARIFA ZINGINE ZA MWANAFUNZI.

i. ULEMAVU (Ngozi, miguu, mikono n.k).....
ii. UGONJWA (Kifafa nk) ……
iii. Je, baba ni hai?.....
iv. Je, mama ni hai?.....
v. Je, baba na mama wanaishi pamoja?.....

Nakiri kuwa taarifa niliyojaza hapo juu ni ukweli mtupu kwa mujibu wa uelewa wangu.

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO.

LUDEWA DISTRICT COUNCIL
MAVALA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 789 NJOMBE.

DATE.....

A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To medical officer.....

PART A: PERSONAL PARTICULARS AND DIAGNOSIS

Pupils name..... Age.....

Please examine the above pupil as to his/her physical and mental fitness for a full time student in Mavala secondary school. In the incourse of examination please consider the following items.

1. Eye sight.....
2. Hearing (impairment).....
3. Blood pressure.....
4. Asthma.....
5. Urine for sugar .....
6. Skin disease .....
7. Neurosis .....
8. Venereal .....
9. Pregnancy .....
10. Other serious diseases .....

Part B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by medical officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission into a secondary school.
2. Other comments

.....

.....

Full name .....

Signature..... Date .....

Designation ..... Official stamp .....